# UTENGENEZAJI WA VYAKULA VYA KUKU

## MWONGOZO KWA MFUGAJI



RLDC
RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

intercooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

swisscontact

# RLDC na Uboreshaji wa Maisha Vijijini

Shirika la Rural Livelihood Development Company (RLDC ni moja ya mafanikio ya ushirikaiano kati ya Tanzania na Uswisi kwenye mchakato wa kupambana na umaskini na kuboresha maisha ya jamii za vijijini. Hii ni taasisi isiyo ya kibiashara ili yoanzishwa mwaka 2005 na mashirika ya Intercooperation na Swisscontact, lengo kuu likiwa kutekeleza Programu ya kuendeleza maisha ya jamii za vijijini (RLDP). Programu hii inasha bihiana na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini (MKUKUTA). Dhamira kuu ya RLDC ni Kuendeleza/kuboresha mifu mo ya masoko ili kuwawezesha wazalishaji wa vijijini kutumia
fursa zilipo kuboresha maisha yao.

Kwa sasa, RLDC inatelekeleza awamu ya pili ya mpango wake (2008-2011) na inaweka msukumo zaidi kwenye uendelezaji wa mifumo ya masoko. RLDC inafanya kazi katika mikoa sita ya Kanda ya kati-Dodoma, Singida, Morogoro, Shinyanga, Tabora, na Manyara. Jamii nyingi maskini zinaishi katika ukanda huu wenye sehemu kubwa yenye hali ya mvua chache na nusu jangwa inayostawisha shughuli chache za kiuchumi.

Hata hivyo kuna fursa nyingi sana zinazoweza kutoa ajira na kuboresha ya jamii zake. RLDC inafadhiliwa na Serikali ya Uswisi kupitia shirika la Uswisi la maendeleo (SDC).

Kwa sasa RLDC inawezesha sekta  za pamba, alizeti, maziwa, ufugaji wa kuku wa kienyeji, mpunga na habari kupitia vipindi vya redio kwa ajili ya wazalishaji wa vijijini.

**“RLDC inaboresha mifumo ya masoko ili kuwezesha wazalishaji wa vijijini kuinua maisha yao”**

# UTENGENEZAJI WA VYAKULA VYA KUKU

## MWONGOZO KWA MFUGAJI

RLDC
RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

intercooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development
and Cooperation SDC

swisscontact

# YALIYOMO

Mwongozo kwa mfugaji

Utangulizi 1

Jinsi ya kupata virutubisho mbalimbali 2

Mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandaa chakula cha kuku 5

Hifadhi ya vyakula vilivyochanganywa 9

# Utengenezaji wa vyakula vya kuku kwa ajili ya makundi mbalimbali

## Utangulizi



*Mtama*



*Mashudu*



*Dagaa*



*Mchicha*

Ufanisi katika shughuli ya ufugaji wa kuku unategemea mambo mbalimbali kama:

- Ujenzi wa banda bora.
- Uchaguzi wa kuku wazazi wenye sifa nzuri.
- Udhibiti na tiba ya magonjwa mbalimbali.
- Ulishaji bora.

Mwongozo huu unaeleza mambo ya msingi katika kuandaa vyakula vya kuku wa rika tofauti. Kama mifugo wengine, kuku wanahitaji vyakula vyenye virutubisho vyote muhimu vinavyohitajika na mwili kama wanga, protini, Madini, mafuta , vitamin na maji.

# Jinsi ya kupata virutubisho mbalimbali

Ili kifaranga awe na afya nzuri na akue upesi anahitaji chakula maalum. Chakula hicho ni mchanganyiko wa viini lishe mbali mbali. Kila kiini lishe ni lazima kiwe katika kiwango sahihi kulingana na mahitaji ya mwili wa kifaranga. Viini lishe anavyohitaji kifaranga ni:

- Wanga
- Protini
- Madini
- Mafuta
- Vitamini
- Maji

Mchanganyiko sahihi wa viini lishe kwa mahitaji ya kifaranga, humwezesha kukarabati na kujenga mwili (kukua) haraka. Viini lishe tulivyovitaja hapa juu hupatikana katika aina mbali mbali za viungo ghafi vya chakula cha kuku kama ifuatavyo:



*Mtama aina tofauti*



*Mtama aina tofauti*



*Karanga*



*Mahindi*

## Wanga

Wanga hupatikana katika pumba, chenga au dona ya nafaka kama mahindi au mtama aina ya serena, lulu n.k.

# Vyanzo vya Wanga

## Mafuta

Mafuta hupatikana katika mbegu kama karanga au alizeti. Mbegu hizi zikikamuliwa mashudu yake hubaki na kiasi fulani cha mafuta. Haya hutumika kulishia mifugo mbali mbali.



*Alizeti*



*Alizeti*



*Mashudu ya karanga*

## Protini

Kiini lishe hiki hupatikana katika mashudu ya karanga au alizeti, dagaa, damu ya wanyama kama ng'ombe, mbuzi n.k.



*Mashudu*



*Dagaa*

Damu hiyo unaweza kuipata machinjioni. Changanya damu mbichi na pumba katika ndoo au chombo chochote kilicho wazi upande mmoja. Vuruga mchanganyiko huo kwa kipande cha mti, halafu fikicha kwa viganja ili kuondoa mabonge. Sambaza mchanganyiko huu juu ya bati halafu anika juani mpaka ukauke kikamilifu.

**Tahadhari: Ukiamua kutumia damu katika mchanganyiko wa chakula hakikisha utaitumia mfululizo.Maana kuku wakiaasha izoea ikikosekana huanza tabia ya kudonoana.**

Protini hupatikana pia katika unga wa mbegu za jamii ya kunde kama maharage, kunde, soya n.k.

## Madini

Madini aina 'Calcium' (tamka kalshium) na fosforasi hupatikana katika unga wa dagaa na mifupa ya wanyama iliyochomwa na chokaa maalum ya kuku ipatikanayo katika maduka ya pembejeo za kilimo, chumvi, hata na majivu ya kawaida ya jikoni.

## Maandalizi ya unga wa mifupa



*Chumvi*



*Unga wa Mifupa*

Chukua mifupa ya wanyama hasa ile mirefu (ya miguu na mingineyo) ichome moto hadi iive. Utafahamu kuwa imeiva inapokuwa na rangi nyeupe mifupa mizuri zaidi ni ile mirefu yaani ya miguu na mikono kuliko ile ya kichwa ambayo mara nyingi huwa kama mkaa (ambayo haifai). Iache ipoe kabisa halafu itwange hadi isagike iwe unga. Hapo inakuwa tayari kuchangnywa kwenye chakula cha kuku wako.

## Vitamini

Vitamini hupatikana katika majani mabichi ya mti aina ya Lusina, majani ya mpapai, mchicha wa nyumbani au wa prorini.

Vitamini hupatikana pia katika majani mabichi ya mimea ya jamii ya mikunde kama marejea na luseni n.k.ambayo hupendelewa kuliwa na kuku. Unaweza kukausha mimea hiyo kivulini na kuitwanga katika kinu au kufikicha kwa viganja ili kupata unga. Viungo ghafi tulivyovitaja hapa juu hupatikana katika vijiji vingi hapa nchini. Kwa hiyo mkulima unaweza kujitengenezea mwenyewe chakula kinachofaa kwa ajili ya kuku wako.



*Mchicha*

## Mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandaa chakula cha kuku

- Upatikanaji wa malighafi kama:- Mahindi mtama, pumba, nk. Kutegemeana na kinachopatikana katika eneo husika.
- Uchaguzi wa malighafi utategemea uwezo wa mfugaji.
- Utengenezaji wa chakula unategemea rika la kuku unaowatengenezea.
- Kiasi au uwingi wa chakula kitakachotengenezwa kitategemea uwezo wa mfugaji kifedha.
- Mali ghafi zinazotumika kutengenezea chakula ziwe zimekauka vizuri ili kuepuka uwezekano wa kuota ukungu ambao ni hatari kwa afya ya kuku.
- Hata kama mali ghafi ni kavu ikaguliwe kuhakikisha kwamba haina ukungu na iwe haijaoza.

## Matayarisho

- Andaa aina zote za viungo ghafi zilizo bora katika wingi wa kutosha (uzito). Pumba au dona, mashudu n.k. viwe havikuvunda. Tena viwe safi yaani havikuchanganyika na uchafu wowote bila kushambuliwa na wadudu.
- Tayarisha kopo tupu lenye ujazo wa lita 1 kwa ajili ya kupimia.  Mfano wa kopo linalofaa ni lile la Pride, Kimbo au Blue band. Kila kiungo unachotaka kuchanganya pima ujazo wa lita moja ili ujue una uzito gani (waweza kuomba msaada maduka ya jirani wakupimie). Ukiishafahamu hivyo utaweza kupima uzito sahihi wa kuweka kwenye mchanganyika wako. Kwa mfano: Kama lita 1 ya pumba ni nusu kilo, ina maana mahali unapotakiwa kuweka kilo 1 utaweka lita 2 yaani makopo 2 ya lita 1.
- Kama unaandaa kiasi kikubwa cha chakula ni vizuri uwe na mizani ya kutumia kwa ajili ya kuandaa chakula chenye uwiano sahihi. Maana ni rahisi kupoteza hesabu za makopo kama unaandaa chakula kingi.
- Kama mchanganyiko wako wa chakula una dagaa, mahindi au mashudu hakikisha kwamba vitu hivi vinabarazwa mashineni kabla ya kuchanganya (yaani vinavunjwa vunjwa).
- Baraza vyakula hivi upate chembechembe zinazolingana na rika ya kuku unaotaka kulisha chakula unachoandaa.

## Utaratibu wa kuchanganya viungo ghafi

Kwanza pima kwa makopo au mizani viungo ghafi vyote vyenye uzito mkubwa viweke kwenye fungu lake moja na kuvichanganya vizuri. Kwa mfano:

- Unga wa nafaka
- Pumba ya mashudu
- Mashudu ya alizeti

Halafu kwenye fungu la pili changanya vizuri viungo vyenye uzito mdogo kama:

- Unga wa dagaa
- Unga wa mifupa au chokaa
- Chumvi ya jikoni

**Mwishoni** Changanya mafungu yote mawili kikamilifu.

**Kutengeneza chakula cha vifaranga umri wa siku ya kwanza hadi majuma nane (0-8 wiki)**

| **Aina ya vyakula** | **Kiasi (Kilo)** |
|---|---|
| Unga wa nafaka kama mahindi au mtama | 40 |
| Pumba za mtama, mahindi, uwele, | 27 |
| Mashudu ya, alizeti, , ufuta karanga au pamba n.k | 20 |
| Unga wa mifupa au chokaa ya kuku | 2.25 |
| Dagaa au mabaki ya samaki | 10 |
| Chumvi ya jikoni | 0.5 |
| Virutubisho (Premix) | 0.25 |
| **Jumla** | **100** |

**Kutayarisha chakula cha kuku wanaokua (miezi miwili na nusu hadi miezi 5)**

| **Aina ya malighafi** | **Kiasi kinachohitajika kutengeneza michanganyiko mbali mbali ya vyakula (kilo)** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 |
| Mahindi yaliyobarazwa | 45 | 18 | - | - |
| Mtama | 5 | - | 27 | - |
| Mihogo | - | 20 | 10 | 40 |
| Pumba za mahindi | 15 | 15 | 15 | 21 |
| Pumba laini za mpunga | - | - | - | - |
| Pumba za ngano | - | 15 | 15 | 10 |
| Mashudu ya alizeti | 15 | - | - | 16 |
| Mashudu ya pamba | 3 | 5 | - | - |
| Maharage/kunde zilizosagwa | 1 | 5 | 3.5 | 1 |
| Kisamvu | - | - | 4.75 | - |
| Lusina/luseni iliyosagwa | 1 | 5 | 5 | 2 |
| Chokaa | 5 | 6 | 4 | 5 |
| Dagaa/Sangara | 6 | 5 | 5 | - |
| Mifupa iliyosagwa | 2.25 | 2.25 | 2 | 2 |
| Damu iliyokaushwa | - | 1 | 5 | 3.25 |
| Chumvi ya kawaida | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| Vitamini/madini (premix) | 0.25 | 0.25 | 0.25 | 0.25 |
| **Jumla** | **100** | **100** | **100** | **100** |

Namba moja hadi nne katika jedwali hili ni michanganyiko wa vyakula aina 4 tofauti kwa ajili ya kuku wenye umri uliotajwa hapa juu. Ukihitaji kuandaa chakula cha kuku hao, chagua mchanganyiko mmoja (kwa safu wima) wenye malighafi zinazopatikana kwenye eneo lako kwa urahisi na utakazozimudu kifedha.

## UTAYARISHAJI CHAKULA CHA KUKU WANAOTAGA (MIEZI 5 HADI MIEZI 18) PAMOJA NA KUKU WAZAZI

| Aina ya vyakula | Kiasi (kilo) |
|---|---|
| Chenga za Mahindi | 31.5 |
| Mtama | 15.0 |
| Pumba ya mahindi | 13.0 |
| Mashudu ya Alizeti | 20.0 |
| Dagaa | 12.0 |
| Chokaa | 3.0 |
| Premix | 0.25 |
| Chumvi | 5.0 |
| **Jumla** | **100** |

AU

| Aina ya vyakula | Kiasi (kilo) |
|---|---|
| Dagaa kilo | 12.0 |
| Chenga za mahindi | 30.0 |
| Mtama | 6.75 |
| Mashudu | 20.0 |
| Pumba ya mahindi | 23.0 |
| Chumvi | 0.25 |
| Chokaa | 3.0 |
| Mifupa | 5.0 |
| **Jumla** | **100** |

Vyakula hivi vyote vinafaa kwa kuku watagaji na kuku wazazi. Tofauti kwenye kuku wazazi ni kuwa wanalishwa kiasi pungufu ili wasinenepe na kushindwa uzalishaji.

Mwongozo uliotolewa, hapa juu ni kwa ajili ya kuandaa kilo 100 za chakula cha kuku, endapo unataka kutengeneza kilo 500 itabidi kila kilichopo kwenye mchanganyiko kizidishwe, mara tano ndipo kupata hizo kilo 500.

Endapo mfugaji anataka kukutengeneza chini ya kilo 50 hali kadhalika anatakiwa, kupunguza/kugawanya hizo kilo 100 kwa mbili hivyo unapata kilo 50 unazohitaji. Vitu vinavyobarazwa ni Mahindi Dagaa Mashudu na mifupa iliyochomwa ambayo haijasagwa.

Chakula cha vifaranga kiwe laini zaidi kuliko kile cha kuku wakubwa wanaotaga.

Kwa kawaida kuku mmoja mtagaji hula gramu 100 za chakula kwa siku. Wastani wa mahitaji ya kuku 50 kwa siku ni kilo 5.

## Angalizo

Mwongozo huu umeekeze jinsi ya kutengeneza chakula cha kuku kwa rika mbali mbali. Ikumbukwe kuwa aina ya chokaa inayotumika katika utengenezaji wa chakula cha kuku ni chokaa maalum inayopatikana kwenya maduka ya pembejeo za mifugo. Siyo chokaa ya kuchimba chini wala ile itumiwayo kujengea nyumba.

Hifadhi ya vyakula vilivyochanganywa

- Baada ya kuchanganya chakula kijaze kwenye mifuko safi, mikavu isiyokuwa na takataka za aina yoyote na isiyo toboka.
- Hifadhi magunia yako juu ya matofali yaliyopangwa mabanzi juu yake. Hii ni kwa ajili ya kuepuka unyevu unaotoka sakafuni ambao unaoweza kuharibu ubora wa chakula kwa kusababisha ukungu.
- Hakikisha chumba cha kuhifadhia chakula cha kuku kisiruhusu panya kuingia na paa lisivuje.
- Wakati wa kuandaa chakula, weka kumbukumbu ya gharama zote zilizotumika katika kuandaa chakula hicho mfano:

    - Gharama zote za viungo ghafi.
    - Gharama za usafiri wa kwenda kununua visivyo patikana katika mazingira yako.
    - Gharama ya kubaraza viungo ghafi n.k.
    - Gharama ya muda wako wote uliotumia kukusanya mali ghafi na kutengeneza chakula.

- Tunza kumbukukmbu hizi zikusaidie kukadiria bei ya kuuza chakula cha kuku.
- Katika kupanga bei ya kuuza chakula zingatia gharama ya kukiandaa ongezea na faida mtakayokubaliana katika kikundi cha wazalishaji wa chakula.

- Kama kikundi kitakuwa na uwezo wa kifedha, kinashauriwa kinunue mali ghafi wakati wa mavuno ambapo bei zinakuwa nafuu ili kupunguza gharama za uzalishaji na kupata faida kubwa zaidi baadaye.
- Mali ghafi hizi zihifadhiwe vizuri kama chakula kinavyohifadhiwa sawa na livyoelekezwa awali.
- Kikundi kiangalie uwezekano wa kupata mali ghafi sehemu nyingine kwa bei nafuu. Kwa kuzingatia na gharama za usafirishaji.
- Uchanganyaji wa chakula uzingatie mahitaji halisi ya wanakikundi wazalishaji wa kuku, ili kuepuka chakula kilichochanganywa kisikae muda mrefu na kupoteza ubora wake.
- Unapoweka chakula kwenye mifuko weka kwa kipimo maalum ambacho kitasaidia, katika kukadiria bei ya kuuzia na utatumia kipimo hicho hicho kuuza.

**KUMBUKA YAFUATAYO UNAPOKUWA UNAANDAA CHAKULA CHA KUKU**

- Tumia mali ghafi zinazopatikana ndani ya mazingira yako.
- Kumbuka wanakikundi wengine wazalishaji wa kuku wanategemea sana kupata chakula cha kuku wao kutoka kwa waandaaji wa chakula. Hivyo mnatakiwa kuwa makini kutengeneza chakula chenye ubora unaotakiwa kwa kuku.
- Kutozingatia hili kutaharibu mtiririko mzima wa uzalishaji. Maana matokeo yake ni kuku kutaga mayai machache chini ya kiwango kinachotakiwa. Pia hii itaathiri ukuaji wa vifaranga na kuku wanaoendelea kukua .Uuzalishaji kwa jumla utashuka.

RLDC

RURAL LIVELIHOOD
DEVELOPMENT COMPANY

Jengo la NBC
Ghorofa ya Pili, Mtaa wa Nyerere
S.L.P. 2978, Dodoma, Tanzania.
Simu +255 26 2321455, Faksi +255 26 2321457.
Barua pepe: info@rldc.co.tz.
Tovuti: www.rldc.co.tz.